Jarida la Kiswahili Sanifu

Mabadiliko ya Kimofolojia ya Vitenzi vya Kiswahili: Uchunguzi wa Matini Rasmi za Kati ya Mwaka 1870 na 1970

Dickson Mlowezi[1] Michael Mashauri[2]
[1]Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira; Dickson.mlowezi@makumira.ac.tz ORCID 0009-0005-2599-5686
[2]Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; mashauridar@gmail.com ORCID 0009-0001-7058-1694

IKISIRI

Makala hii inachunguza mabadiliko ya kimofolojia ya vitenzi vya Kiswahili katika matini zilizochapishwa kati ya mwaka 1870 na 1970 ili kubainisha mabadiliko ya viambishi vya kabla na baada ya mzizi. Utafiti ulitumia mkabala wa kitaamuli na uchanganuzi wa matini. Matoleo ya magazeti tisa yaliteuliwa kwa usampulishaji nasibu tabakishi; *Orodha ya Msamiati* ya Steere (1870) pia ilitumika. Vitenzi 68 vilinakiliwa, vikalinganishwa na maumbo ya Kiswahili sanifu na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika ya Kiparsky (1982). Matokeo yanaonesha mabadiliko katika viambishi vya kiima, njeo, yambwa, urejeshi na viambishi tamati. Mabadiliko hayo yanajumuisha {twa-}, {mwa-} na {wa-} kuwa {tu-}, {m-} na {u-}; kuimarika kwa {-na-} ya wakati uliopo; kubadilika kwa {mw-} kuwa {mu-} mbele ya /u/; kufinyika kwa matumizi ya {-eni} na {-ni}. Makala inahitimisha kuwa mabadiliko hayo yanaakisi upangaji upya, urahisishaji na usanifishaji wa mfumo wa kimofolojia wa vitenzi. Inapendekeza kuundwa kwa korpasi ya matini za kihistoria na kufanyika kwa tafiti kuhusu mabadiliko katika viwango vya lugha na lugha nyingine za Kibantu.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:
Mabadiliko ya Maumbo, Matini Rasmi, Mofolojia Leksika, Vitenzi vya Kiswahili

Historia ya Makala:
Tarehe ya Kutumwa:11Juni 2026
Tarehe ya Kurekebishwa:02 Sept 2026
Tarehe ya Kukubalika:11 Sept 2026
Mtandaoni: 09 Oktoba 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: +255676734412; *Barua Pepe* dickson.mlowezi@makumira.ac.tz

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Mlowezi, D. & Mashauri, M. (2026). Mabadiliko ya Kimofolojia ya Vitenzi vya Kiswahili: Uchuguzi wa Matini Rasmi za kati ya Mwaka 1870 na 1970: 3(2), 88-98

© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

1.0 Utangulizi

Mofolojia ya vitenzi vya Kiswahili ni eneo muhimu kwa kuwa uchunguzi unahusu mabadiliko ya maumbo ya vitenzi katika kipindi cha kati ya mwaka 1870 na 1970. Kitenzi cha Kiswahili hujengwa kwa vipashio mbalimbali vinavyojitokeza kabla na baada ya mzizi. Vipashio hivyo ni pamoja na viambishi vya kiima, njeo, hali, ukanushi, yambwa, urejeshi, mzizi, viambishi vya kauli na irabu ya mwisho.

Polome (1967) na Wesana-Chomi (2013) wanaeleza kuwa shina la kitenzi huwa na mzizi ambao unaweza kuambatana na kiambishi kimoja au zaidi. Kitenzi cha Kiswahili huwa na irabu ya mwisho, ambayo mara nyingi ni {-a}. Polome (1967) anaongeza kuwa irabu hii ya mwisho inaweza kubadilika, hususan pale kitenzi kinapokuwa katika hali ya ukanushi. Ud Deen (2005) anaeleza kuwa muundo wa kitenzi cha Kiswahili hujumuisha viambishi vya kiima, viambishi vya njeo, viambishi vya ukanushi, viambishi vya yambwa, mzizi, viambishi vya kauli na irabu ya mwisho. Kitenzi cha Kiswahili ni kipashio changamani kinachoweza kubeba taarifa nyingi za kisarufi ndani ya neno moja. Petzell (2005) anaeleza kuwa muundo wa vitenzi vya Kiswahili hujumuisha kiambishi awali, kiambishi cha njeo, kiambishi cha urejeshi, kiambishi cha yambwa, mzizi na viambishi vya unyambulishi au upanuzi wa kitenzi. Viambishi vya upanuzi wa kitenzi huweza kuonesha kauli kama vile usababishi, utendeka na utendana. Mabadiliko yoyote katika nafasi au matumizi ya viambishi yanaweza kuathiri muundo mzima wa kitenzi. Schönhof-Wilkans (2012) anaeleza kuwa mfumo wa uambishaji wa vitenzi vya Kiswahili ni changamani kwa sababu mahusiano mengi ya kisarufi hudhihirishwa kupitia viambishi. Viambishi hivyo huweza kuonesha mtenda, njeo, hali, yambwa na dhamira. Schönhof-Wilkans (2012) anaendeleza hoja hii kwa kutofautisha vitenzi elekezi na vitenzi sielekezi. Vitenzi elekezi huhitaji au huruhusu kuwapo kwa nomino inayopokea athari ya tendo, yaani yambwa (tendwa), kama katika sentensi *Asha amesoma kitabu*, ambapo *kitabu* ndicho kilichotendwa. Baadhi ya vitenzi vilivyopokea kauli ya kutendea vinaweza kuwa na yambiwa (tendewa) pamoja na yambwa. Katika sentensi *Asha amemwandikia Juma barua*, *barua* ni yambwa kwa sababu ndiyo iliyoandikwa, ilhali *Juma* ni yambiwa kwa sababu ndiye aliyetendewa tendo la kuandikiwa. Kinyume chake, vitenzi sielekezi havihitaji yambwa, kama katika *mtoto amelala*. Ufafanuzi huu unaonesha kuwa mabadiliko ya viambishi vya yambwa na vya kauli, kama *-m-* katika *amemwandikia* na *-i-* katika *-andikia*, yanaweza kuathiri muundo na uhusiano wa kisarufi baina ya kitenzi na nomino zinazoandamana nacho. Tafiti hizi zinathibitisha umuhimu wa kuchunguza nafasi na dhima za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili.

Wesana-Chomi (2017), kama Polome (1967) na Ud Deen (2005) wanavyosema, anasisitiza kuwa muundo wa kitenzi cha Kiswahili unaweza kueleweka kwa kuchunguza vipashio vinavyokijenga kitenzi na nafasi ya irabu ya mwisho {-a}. {-a} ni kiambishi tamati kinachojitokeza mwishoni mwa vitenzi vingi vya Kiswahili. Hoja hii ni muhimu kwa makala hii kwa sababu baadhi ya mabadiliko yanayochunguzwa yanahusu viambishi vinavyojitokeza baada ya mzizi wa kitenzi. Hakimu (2020) anaeleza kuwa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu navyo hujengwa kwa viambishi vya kabla na baada ya mzizi. Ingawa utafiti wake ulijikita katika ubantuishaji wa vitenzi vyenye asili ya Kiarabu, maelezo yake yanasaidia kuthibitisha kuwa muundo wa kitenzi cha Kiswahili unaweza kuchunguzwa kwa kuzingatia mpangilio wa viambishi kabla na baada ya mzizi.

Kwa kuzingatia mawazo ya watafiti hawa, makala hii inachukulia kitenzi cha Kiswahili kama muundo unaojengwa kwa viambishi vya kabla ya mzizi na viambishi vya baada ya mzizi. Viambishi vya kabla ya mzizi ni pamoja na kiambishi awali tangulizi, kiambishi cha kiima, kiambishi cha ukanushi, kiambishi cha njeo, kiambishi cha yambwa, kiambishi cha urejeshi na kiambishi cha kujirejea. Kwa upande mwingine, viambishi vya baada ya mzizi ni pamoja na viambishi vya kauli za vitenzi, irabu ya mwisho na baadhi ya viambishi tamati vya ziada.

Katika makala hii, dhana ya viambishi vya kabla na baada ya mzizi imetumika kama msingi wa kuchambua mabadiliko ya maumbo ya vitenzi vya Kiswahili katika kipindi cha 1870 hadi 1970. Uchunguzi umezingatia namna viambishi fulani vilivyobadilika, kupungua matumizi, kuhama nafasi au kubadilisha dhima yake ya kisarufi katika Kiswahili sanifu cha baadaye. Kwa mfano, matumizi ya kiangami {-ni} katika maumbo kama *atapata-ni? amefanya-ni? wataka-ni?*, *walia-ni?* na *nawaambia-ni?* yanaonesha mojawapo ya vipengele vya kihistoria vinavyodhihirisha mabadiliko ya kimofolojia katika vitenzi vya Kiswahili.

2.0 Suala la Utafiti

Suala la mabadiliko ya maneno si geni katika lugha ya Kiswahili. Kama ilivyo kwa lugha nyingine, Kiswahili kimepitia mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki kutokana na matumizi yake katika vipindi tofauti vya kihistoria. Mwaro-Were (2001) anaeleza kuwa

baadhi ya maneno ya zamani ya Kiswahili bado yanapatikana katika maandiko ya kale, ingawa hayatumiki sana katika maandishi ya kila siku ya Kiswahili cha sasa. Maneno hayo hupatikana katika kamusi za zamani, magazeti ya kale na kazi za fasihi ya Kiswahili kama vile *Utenzi wa Tambuka* wa mwaka 1649 au 1650, *Utenzi wa Mwanakupona*, *Al-Inkishafi* wa mwaka 1810 hadi 1820, pamoja na mashairi ya washairi kama M. H. Mbega, A. N. J. Bhalo, Muyaka na Fumo Liyongo.

Hoja ya msingi inayojitokeza katika maelezo ya Mwaro-Were (2001) ni kwamba maandiko ya zamani ya Kiswahili yana hazina kubwa ya taarifa za kisarufi ambazo hazijachunguzwa kikamilifu katika Kiswahili cha sasa. Hivyo, uchunguzi wa maandiko hayo unaweza kusaidia kubainisha namna lugha ya Kiswahili ilivyobadilika hasa katika mofolojia ya vitenzi katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Kwa kuzingatia msingi huo, makala hii inachunguza mabadiliko ya maumbo ya vitenzi vya Kiswahili katika matini rasmi za kati ya mwaka 1870 na 1970. Mwaka 1870 umechaguliwa kuwa mpaka wa mwanzo kwa sababu unaashiria kipindi ambacho matumizi ya hati ya Kirumi katika uandishi wa Kiswahili yalianza kuimarika. Mwaka 1970 umechaguliwa kuwa mpaka wa mwisho kwa sababu unaashiria kuvunjwa rasmi kwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki na kuanzishwa kwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), hatua iliyofungua awamu nyingine ya usanifishaji na ukuzaji wa Kiswahili (Hans, 2017). Kwa hiyo, kipindi cha 1870 hadi 1970 kinafaa kuchunguzwa kwa kuwa kinawakilisha awamu muhimu ya uandishi, usanifishaji na mabadiliko ya kimofolojia ya Kiswahili.

2.0 Mapitio ya Maandishi

Mabadiliko ya maneno katika Kiswahili yamejadiliwa na watafiti mbalimbali kwa mitazamo tofauti. Baadhi ya watafiti wamejikita katika mabadiliko ya maneno katika Kiswahili sanifu, kwa mfano Ngonyani (2006). Wengine wamechunguza mabadiliko ya maneno katika lahaja mbalimbali za Kiswahili, wakiwemo Nurse na Hinnebusch (1993) na Kipacha (2005). Aidha, baadhi ya tafiti zimeangalia mabadiliko ya maneno ya Kiswahili kwa kuzingatia athari za lugha za kigeni kama Kiarabu na Kiingereza. Miongoni mwa tafiti hizo ni Babusa (2019), Batibo (2002), Gibson na wenzake (2019), Gichuru (2020), Hakimu (2020, 2023), Hussein (2016) na Shembilu (2015). Kwa ujumla, tafiti hizi zimetoa mchango muhimu katika kueleza mabadiliko ya maneno, lahaja, ukopaji wa msamiati na mabadiliko ya maana katika Kiswahili. Hata hivyo, kuna upungufu wa uchunguzi mahsusi unaobainisha namna maumbo ya vitenzi vya Kiswahili yalivyobadilika katika matini rasmi za kipindi cha 1870 hadi 1970. Pengo hili ndilo linaloshughulikiwa katika makala hii kwa kuchunguza mabadiliko ya viambishi vinavyojitokeza kabla na baada ya mzizi wa kitenzi.

3.0 Methodolojia za Utafiti

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kitaamuli kubainisha na kufasiri mabadiliko ya kimofolojia ya vitenzi vya Kiswahili katika matini za kihistoria. Data zilikusanywa katika maktaba, makumbusho na makavazi ya Dar es Salaam na Dodoma, yanayohifadhi machapisho muhimu ya historia ya Kiswahili. Matini zilizochunguzwa ni *Orodha ya Msamiati* ya Steere (1870) na magazeti tisa: *Msimulizi* (1888-1914), *Kiongozi* (1904-1916), *Pwani na Bara* (1910-1916), *Mambo Leo* (1923-1950), *Habari za Leo* (1945-1956), *Umoja* (1947-1962), *Bendera ya Kristo* (1947-1954), *Mwafrika* (1957-1965) na *Lengo* (1964-1970).

Vyanzo hivi viliwakilisha vipindi tofauti vya matumizi rasmi ya Kiswahili. Usampulishaji nasibu tabakishi ulitumika kuteua matoleo ya magazeti. Kila gazeti lilichukuliwa kuwa tabaka moja. Matoleo yaliyopatikana katika kila tabaka yaliorodheshwa kulingana na mwaka wa uchapishaji na kupewa namba, kisha matoleo ya kuchunguzwa yaliteuliwa kwa nasibu. Pale ambapo matoleo yaliyohifadhiwa yalikuwa machache, matoleo yote yaliyopatikana, kusomeka na kuwa na taarifa kamili za uchapishaji yalijumuishwa. Jumla ya kurasa 620 zilichambuliwa. Utaratibu huo ulihakikisha uwakilishi wa vyanzo katika kipindi kilichochunguzwa, licha ya tofauti za upatikanaji wa matoleo.

Uchanganuzi wa matini ulibainisha vitenzi vyenye tofauti za umbo, mpangilio au matumizi ya viambishi vya kabla na baada ya mzizi. Kila kitenzi kilinakiliwa pamoja na gazeti, tarehe, ukurasa na muktadha. Awali, magazeti yalitoa vitenzi 254: *Msimulizi* 12, *Kiongozi* 36, *Pwani na Bara* 29, *Mambo Leo* 67, *Habari za Leo* 18, *Umoja* 24, *Bendera ya Kristo* 52, *Mwafrika* 2 na *Lengo* 14. Baada ya kuondoa marudio, vilibaki vitenzi 61 na 7 kutoka kwa Steere (1870) na kufanya jumla ya vitenzi 68.

Aidha, ulinganishi wa maumbo ya vitenzi haukufanywa kwa kutumia matoleo ya baada ya mwaka 1970 ya magazeti yaleyale, kwa kuwa baadhi yake yalikoma kuchapishwa kabla ya mwaka huo au kufikia mwaka 1970. Badala yake, maumbo yaliyobainishwa katika vyanzo hivyo yalilinganishwa na maumbo yanayotumika katika Kiswahili cha sasa. Katika kufanya ulinganishi na kufasiri data, mtafiti alitumia umahiri wake wa Kiswahili kama lugha ya kwanza pamoja na maarifa

yake ya kitaaluma katika isimu ya Kiswahili. Aidha, ili kupunguza utegemezi wa uamuzi binafsi wa mtafiti na kuongeza uthabiti wa uchanganuzi, maumbo ya sasa yalithibitishwa kwa kurejelea maandiko ya kisasa ya Kiswahili.

4.0 Nadharia ya Mofolojia Leksika

Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika, nadharia inayotambua mofolojia kama kiwango muhimu cha uchanganuzi wa lugha. Nadharia hii iliibuka kutokana na haja ya kueleza uundaji wa maneno kwa kuzingatia uhusiano kati ya mofolojia, fonolojia na leksikoni. Wataalamu kama Aronoff (1976), Katamba na Stonham (2018), Kiparsky (1982) na Lieber (1992) wanaeleza kuwa uundaji wa maneno hauwezi kufafanuliwa kikamilifu kwa kutegemea sintaksia au fonolojia pekee, bali unahitaji kuchunguza nafasi, mpangilio na dhima ya mofimu ndani ya neno. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kuwa neno huundwa kwa hatua maalumu ndani ya leksikoni. Katika mchakato huo, viambishi hupachikwa kabla au baada ya mzizi kulingana na kanuni za kimaumbo na kifonolojia za lugha husika. Kwa mujibu wa Kiparsky (1982), kila kiambishi kinapaswa kuelezwa kwa kuzingatia mahali kinapopachikwa, kazi yake ya kisarufi na sifa za umbo linalozalishwa baada ya upachikaji huo.

Nadharia ya Mofolojia Leksika imejengwa katika mihimili ya uamilifu wa sheria mahususi za kisarufi. Mihimili hiyo ni kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya kuhifadhi muundo, kanuni ya ufinyu wa sifa na mhimili wa kwingineko. Katika makala hii, mihimili miwili imetumika kuchambua mabadiliko ya maumbo ya vitenzi vya Kiswahili katika matini rasmi za kati ya mwaka 1870 na 1970. Mihimili hii ni kanuni ya ngazi leksika na kanuni ya ufinyu wa sifa. Mihimili hii imesaidia kubainisha mabadiliko ya nafasi na dhima za viambishi vya kabla na baada ya mzizi, hususan viambishi vya kiima, njeo, yambwa, urejeshi na viambishi tamati. Hivyo, nadharia hii imesaidia kueleza kuwa mabadiliko ya vitenzi vya Kiswahili hayahusu maumbo pekee, bali upangaji upya pia wa vipashio vya kisarufi ndani ya kitenzi. Kwa msingi huu, nadharia imefaa kuonesha uhusiano kati ya mageuzi ya kimuundo na uthabiti wa mfumo wa vitenzi katika Kiswahili kwa matumizi rasmi na ya kitaaluma.

5.0 Mabadiliko ya Maumbo ya Vitenzi vya Kiswahili cha kati ya Mwaka 1870 hadi 1970

Sehemu hii inachambua mabadiliko ya maumbo ya vitenzi vya Kiswahili kati ya mwaka 1870 hadi 1970. Data inaonesha kuwa mabadiliko hayo yalihusu viambishi vya kabla na baada ya mzizi. Mabadiliko haya yalihusu viambishi vya kabla ya mzizi ni kiambishi awali tangulizi (KAT), cha njeo (NJ) na cha yambwa (YA). Viambishi vya baada ya mzizi ni urejeshi (UR) na viambishi tamati vya wingi (KTZ). Mabadiliko hayo yanaonesha upangaji upya wa mfumo wa kimofolojia wa Kiswahili. Maelezo yafuatayo yanaonesha mabadiliko ya viambishi hivyo.

5.1 Mabadiliko ya Viambishi Awali vya Kiima katika Vitenzi

Uchunguzi wa makala hii unaonesha kuwa vitenzi vya Kiswahili vya kati ya mwaka 1870 hadi 1970 vilikuwa na baadhi ya viambishi vya kiima ambavyo vimebadilika katika Kiswahili cha baada ya mwaka 1970. Mabadiliko haya yanajitokeza hasa katika nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi, na nafsi ya pili umoja. Katika data zilizochunguzwa, kiambishi {twa-} kilitumika kuonesha nafsi ya kwanza wingi, kiambishi {mwa-} kilitumika kuonesha nafsi ya pili wingi, na kiambishi {wa-} kilitumika katika baadhi ya mazingira kuonesha nafsi ya pili umoja. Katika Kiswahili cha baada ya mabadiliko, nafasi za viambishi hivyo zimechukuliwa na {tu-}, {m-} na {u-}. Jedwali 1 hapo chini unafafanua kwa kina mabadiliko haya.

Na	Kabla ya Mabadiliko	Baada ya Mabadiliko
i	**Twa**-weza	**Tu**-naweza
ii	**Twa**-soma	**Tu**-soma
iii	**Twa**-mpeleka	**Tu**-nampeleka
iv	**Twa**-sema	**Tu**-nasema
v	**Twa**-mwona	**Tu**-namwona
vi	**Twa**-kuomba	**Tu**-nakuomba
vii	**Twa**-waletea	**Tu**-nawaletea
viii	**Twa**-penda	**Tu**-napenda
ix	**Mwa**-niona	**M**-naniona
x	**Mwa**-imba	**M**-naimba
xi	**Mwa**-mngoja	**M**-namngoja
xii	**Mwa**-jua	**M**-najua
xiii	**Mwa**-fahamu	**M**-nafahamu
xiv	**Wa**-taka	**U**-nataka
xv	**Wa**-lia	**U**-nalia
xvi	**Wa**-kimbilia	**U**-naikimbilia
xvii	**Wa**-andika	**U**-naandika
xviii	**Wa**-zalisha	**U**-nazalisha

Jedwali 1: Mabadiliko ya viambishi awali vya Kiima katika kitenzi

Chanzo: *Mambo Leo* (Januari, 1923:2 na 6; 1925:3, 15, 1931:4 na 5, Disemba 1953:3), *Kiongozi* (1906:4, Agosti 1908:1), *Bendera ya Kikristo* (Februari 1954:2) na *Umoja* (Mei 1962:3).

Data katika Jedwali 1 inaonesha matumizi ya maumbo *twa-*, *mwa-* na *wa-* katika kuashiria nafsi katika vitenzi vya wakati uliopo. Maumbo yenye *twa-* yalitumiwa kwa nafsi ya kwanza wingi, *mwa-* kwa nafsi ya pili wingi na *wa-* kwa nafsi ya pili umoja. Kwa mfano, *twaweza*, *twasoma* na *twasema* yanalingana na *tunaweza*, *tunasoma* na

tunasema katika Kiswahili sanifu cha sasa. Vilevile, *mwaimba* na *mwajua* yanalingana na *mnaimba* na *mnajua*, ilhali *wataka* na *waandika* yanalingana na *unataka* na *unaandika*. Kwa kuwa maumbo haya yamepatikana katika magazeti manne yaliyochapishwa katika miaka na mazingira tofauti, kujirudia kwake katika vyanzo mbalimbali kunadokeza kuwa yalikuwa sehemu ya desturi pana ya Kiswahili kilichoandikwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, data za maandishi pekee hazitoshi kuthibitisha kuwa wazungumzaji wote walitumia maumbo hayo katika mazungumzo. Kwa hiyo, hitimisho linahusu matumizi katika matini rasmi zilizochunguzwa, si matumizi ya jamii nzima ya Waswahili. Mfano wa uchanganuzi wake hujitokeza kama ifuatavyo:

[weza]T
[twa[weza]] T, wingi, Po, Nfs1
[[tu[[na[weza]]] T, wingi, Po, Nfs1: Ubadilishaji wa {twa-} kuwa {tu-} na ujitokezaji wa {-na-}
“tunaweza”

Aidha, data inaonesha kuwa kiambishi {mwa-} kilitumika kuashiria nafsi ya pili wingi katika wakati uliopo. Mifano kama *mwa-niona*, *mwa-imba*, *mwa-mngoja*, *mwa-jua* na *mwa-fahamu* inaonesha matumizi ya kiambishi hiki kabla ya mzizi wa kitenzi. Katika Kiswahili cha baada ya 1970, kiambishi hiki kimefupishwa na kuwa {m-}, kama inavyoonekana katika maumbo *m-na-niona*, *m-na-imba*, *m-na-mngoja*, *m-na-jua* na *m-na-fahamu*. Hivyo, mabadiliko kutoka {mwa-} kwenda {m-} yanaweza kuelezwa kama mchakato wa ufupishaji wa kimaumbo na kifonolojia ambao haukubadili dhima ya kisarufi ya kiambishi hicho, bali ulibadili umbo lake. Uchanganuzi wake ni kama ifuatavyo:

[ona]T
[mwa[ni[ona]]] T, wingi, Po, Nfs2
[m[na[ni[ona]]]] T, wingi, Po, Nfs2: Ubadilishaji wa {mwa-} kuwa {m-} na ujitokezaji wa {-na-}
“mnaniona”

Vilevile, data inaonesha kuwa kiambishi {wa-} kilitumika katika baadhi ya mazingira kuashiria nafsi ya pili umoja katika wakati uliopo. Mifano kama *wa-taka*, *wa-lia*, *wa-kimbilia*, *wa-andika* na *wa-zalisha* inaonesha matumizi hayo. Katika Kiswahili cha baada ya mabadiliko, nafasi hii imechukuliwa na kiambishi {u-}, kama inavyoonekana katika maumbo *u-na-taka*, *u-na-lia*, *u-na-kimbilia*, *u-na-andika* na *u-na-zalisha*. Ni muhimu kutofautisha matumizi haya ya kihistoria ya {wa-} kama nafsi ya pili umoja na matumizi ya {wa-} katika Kiswahili cha baada ya mabadiliko kama kiambishi cha nafsi ya tatu wingi. Uchanganuzi wake ni kama ifuatavyo:

[wataka] T
[wa[taka]] T, umoja, Po
[[u[[na[taka]]] T, umoja, Po: Ubadilishaji wa {wa-} kuwa {u-} na ujitokezaji wa {-na-}
“unataka”

Kwa ujumla, mabadiliko haya yanaonesha kuwa viambishi vya kiima katika Kiswahili vilipitia mabadiliko ya kimaumbo yaliyolenga kurahisisha na kusawazisha mfumo wa uambishaji wa vitenzi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, kila kiambishi kina nafasi maalum katika muundo wa neno. Katika data hii, viambishi {twa-}, {mwa-} na {wa-} vilipachikwa kabla ya mzizi katika Kiswahili cha kati ya mwaka 1870 hadi 1970. Katika Kiswahili cha kipindi cha baada ya mwaka 1970, nafasi hizo zimechukuliwa na {tu-}, {m-} na {u-}, huku {-na-} kikichukua nafasi ya kiambishi cha njeo kati ya kiambishi cha kiima na mzizi. Hivyo, mabadiliko haya yanaonesha si tu kubadilika kwa maumbo ya viambishi, bali kuimarika pia kwa mpangilio wa vipashio vya kitenzi katika Kiswahili.

5.2 Mabadiliko ya Matumizi ya Kiambishi cha Njeo ya Wakati Uliopo

Makala hii inaonesha kuwa katika Kiswahili cha kati ya mwaka 1870 na 1970, kiambishi cha njeo ya wakati uliopo hakikujitokeza kwa umbo bayana katika vitenzi. Hata hivyo, baada ya mwaka 1970, kiambishi {-na-} kilianza kutumika kwa uwazi na uthabiti kuonesha tendo linaloendelea kufanyika. Kiambishi hiki kilipata nafasi mahsusi katika muundo wa kitenzi, kikijitokeza baada ya kiambishi cha kiima na kabla ya mzizi. Mabadiliko hayo yalirasimisha mpangilio wa vipashio vya kimofolojia, yakapunguza utegemezi wa kiambishi cha kiima katika kubeba taarifa ya njeo, na kuongeza uwazi wa kisarufi katika uchambuzi wa vitenzi. Mabadiliko haya yanaoneshwa kwa kina katika Jedwali 2 (i-xx) hapa chini.

Na	**Kabla Mabadiliko**	**Kutokuabainika kwa Njeo**	**Baada ya Mabadiliko**
i	**Twa**-weza	**Twa-Ø**-weza	**Tu-na**-weza
ii	**Twa**-soma	**Twa-Ø**-soma	**Tu-na**-soma
iii	**Twa**-mpeleka	**Twa-Ø**-mpeleka	**Tu-na**-mpeleka
iv	**Twa**-sema	**Twa-Ø**-sema	**Tu-na**-sema
v	**Mwa**-niona	**Mwa-Ø**-niona	**M-na**-niona
vi	**Mwa-**imba	**Mwa-Ø**-imba	**M-na**-imba
vii	**Mwa-**mngoja	**Mwa-Ø**-mngoja	**M-na**-mngoja
viii	**Mwa-**jua	**Mwa-Ø**-jua	**M-na**-jua
ix	**Wa**-taka	**Wa-Ø**-taka	**U-na**-taka
x	**Wa**-lia	**Wa-Ø**-lia	**U-na**-lia

xi	**Wa-** kimbilia	**Wa-Ø**-kimbilia	**U-na-** ikimbilia
xii	**Wa-**andika	**Wa-Ø**-andika	**U-na-** andika
xiii	Wa-taka	Wa-**Ø**-taka	Wa-**na-**taka
xiv	Wa-lia	Wa-**Ø**-lia	Wa-**na**-lia
xv	Wa-kimbilia	Wa-**Ø**-kimbilia	Wa-**na-**ikimbilia
xvi	Wa-andika	Wa-**Ø**-andika	Wa-**na-**andika
xvii	A-jiona	A-**Ø**-jiona	A-**na**-jiona
xviii	A-semaje	A-**Ø**-semaje	A-**na-**semaje
xix	A-penda	A-**Ø**-penda	A-**na-**penda
xx	A-wapenda	A-**Ø**-wapenda	A-**na-**wapenda

Jedwali 2*: Mabadiliko ya Matumizi ya Kiambishi cha Njeo ya Wakati Uliopo*.

Chanzo: *Bendera ya Kikristo*, (Novemba 1947:5; Februari 1952:7; Februari 1954:2), *Kiongozi*, (Agosti 1908:1, 2 na 4; Oktoba 1913:4), *Lengo*, (Januari 1968:9), *Mambo Leo*, (Januari 1923:2; Februari 1925:5, 7; Machi 1931:3, 4 na 5; Disemba 1953:3) na *Pwani na Bara*, (Januari 1911:4).

Data katika Jedwali 2 inaonesha kuwa kati ya mwaka 1870 na 1970, baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vilitumiwa bila kiambishi cha njeo ya wakati uliopo {-na-}. Maumbo kama *twa-weza*, *twa-soma*, *mwa-imba*, *mwa-jua*, *wa-taka*, *wa-lia*, *a-jiona* na *a-penda* yalitegemea muktadha kubainisha wakati uliopo. Baada ya mwaka 1970, kiambishi {-na-} kiliingizwa kati ya kiambishi cha kiima na mzizi, hivyo *twa-weza*, *mwa-imba*, *wa-taka* na *a-penda* yakawa *tu-na-weza*, *m-na-imba*, *u-na-taka* na *a-na-penda*. Katika baadhi ya maumbo, kuongezwa kwa {-na-} kuliambatana na kubadilika kwa viambishi vya kiima, ilhali katika *a-penda* kuwa *a-na-penda* na *a-wapenda* kuwa *a-na-wapenda*, kiambishi cha kiima hakikubadilika. Mabadiliko haya yanaonesha kuimarika kwa {-na-} na kusawazishwa kwa muundo wa vitenzi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, uchanganuzi wake ni kama ifuatavyo:

[jua]T
[mwa[ø[jua]]T, wingi, Po, Nfs2
[m[na[jua]]]T, wingi, Po, Nfs 2: Ubadilishaji wa {mwa-} kuwa {m-} na ujitokezaji wa {-na-}
“mnajua”

Kwa ujumla, matumizi ya kiambishi {-na-} katika Kiswahili cha baada ya 1970 yameongeza uwazi wa kisarufi katika kubainisha wakati wa tendo. Mabadiliko haya yanaonesha kuwa mfumo wa vitenzi vya Kiswahili umeendelea kusawazika kwa kuweka alama dhahiri za njeo katika nafasi zinazotabirika. Kwa msingi huo, kuibuka na kuimarika kwa {-na-} ni mojawapo ya vielelezo muhimu vya mabadiliko ya kimofolojia katika vitenzi vya Kiswahili.

5.3 Mabadiliko ya Matumizi ya Kiambishi cha Yambwa {Mw-} kuwa Kiambishi {Mu-} katika Vitenzi vyenye Mfuatano wa Irabu /u/

Baada ya kuchunguza mabadiliko yaliyohusu viambishi vya kiima na njeo, sehemu hii inachanganua mabadiliko ya kiambishi cha yambwa. Data zinaonesha kuwa katika Kiswahili cha kipindi cha 1870 hadi 1970 kulikuwa na mwelekeo wa kifonolojia wa matumizi ya kiyeyusho /w/ kufuatana na irabu /u/ katika mpaka wa mofimu, na hivyo kuunda kiambishi {mw-}. Hata hivyo, matokeo ya utafiti wa makala hii unaonesha kuwa katika Kiswahili cha baada ya mwaka 1970, kulijitokeza mwelekeo mpya ambapo irabu /u/ mbili zilifuatana moja kwa moja katika mpaka wa mofimu, na hivyo kuunda kiambishi cha yambwa {mu-}. Hivyo, mabadiliko yanayohusika hapa si kubadilika kwa dhima ya kisarufi ya kiambishi, kwa kuwa bado kinawakilisha yambwa, bali ni kubadilika kwa umbo lake la kifonolojia kutoka {mw-} kwenda {mu-} katika mazingira ya mzizi unaoanza kwa /u/. Jedwali 3 hapa chini linaonesha.

Na	**Kabla ya Mabadiliko**	**Baada ya Mabadiliko**
i	Ku-**mw**-uliz-a	Ku-**mu**-uliz-a
ii	Ku-**mw**-umiz-a	Ku-**mu**-umiz-a
iii	Ku-**mw**-uguz-a	Ku-**mu**-uguz-a
iv	Ku-**mw**-umbua	Ku-**mu**-umbua
v	**Mw**-uuzie	**Mu**-uzie
vi	Tu-**mwu**-lie	Tu-**mu**-ulie
vii	Ali-**mwu**-a	Ali-**mu**-ua

Jedwali 3: Mabadiliko ya Matumizi ya Kiambishi cha Yambwa {Mw-} kuwa Kiambishi {Mu-} katika Vitenzi vyenye Mfuatano wa Irabu /u

Chanzo: *Habari za Leo* (Disemba 1949:3 na Agosti 1951:1), *Kiongozi* (Aprili 1906:2, 3 na Januari 1910:4), *Mambo Leo* (Januari 1923:7, Februari 1925:5) na *Msimulizi* (Oktoba 1890:3).

Data katika Jedwali 3 inaonesha kuwa katika Kiswahili cha mwaka 1870 hadi 1970, kiambishi {mw-} kilitumika kuwakilisha umoja katika vitenzi vyenye mizizi inayoanza kwa irabu /u/. Matumizi hayo yalitokana na mwingiliano wa kifonolojia kati ya kiyeyusho /w/ na irabu /u/, uliotokeza umbo {mw-}. Hata hivyo, baada ya mwaka 1970, mfuatano wa /w/ + /u/ uliacha kutumika; kiyeyusho /w/ kikaondolewa na irabu /u/ ikajitokeza moja kwa moja. Hivyo, kiambishi {mu-} kikachukua nafasi ya {mw-}, hatua iliyoendana na kanuni za kifonolojia na sarufi ya Kiswahili cha kisasa.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, hususan mhimili wa ufinyu wa sifa, kipashio cha

kimaumbo hubadilika kinapokosa ulinganifu na sifa bainifu za mazingira yake ya kifonolojia. Kwa hiyo, {mw-} kilipoteza uhalali katika mizizi inayoanza kwa /u/ na nafasi yake kuchukuliwa na {mu-}, linaloafikiana na kanuni za fonotaktiki. Mbaabu (2007), anaeleza kuwa {mw-} mbele ya /u/ halifuati kanuni za Kiswahili na linapaswa kurekebishwa kuwa {mu-}, kama ilivyofanyika katika Biblia na Kitabu cha Maombi. Besha (1994) pia anakosoa maumbo kama *mwuaji* na *mwungwana* kwa kutokidhi kanuni zinazokubalika. Hivyo, mabadiliko kutoka {mw-} kwenda {mu-} yanaakisi urahisishaji, usanifishaji na uimarishaji wa mfumo wa kimofolojia wa Kiswahili cha kisasa katika matumizi rasmi zaidi.

5.4 Mabadiliko ya Viambishi Tamati vya Vitenzi vya Kiswahili cha kati ya Mwaka 1870 hadi 1970

Sehemu hii imejikita katika kuchambua viambishi tamati vya vitenzi vya Kiswahili vilivyotumika katika kipindi cha kati ya mwaka 1870 hadi 1970, ambavyo vimebainishwa kuonesha mabadiliko ya kimaumbo katika mpangilio na matumizi yake. Uchambuzi huu ulilenga kufafanua jinsi mabadiliko hayo yalivyojitokeza katika muundo wa vitenzi, hususan katika vipashio vinavyojitokeza mwishoni vinavyoonesha dhima mbalimbali za kisarufi kama vile kuonesha wingi, urejeshi na kuuliza swali. Kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Mofolojia Leksika, sehemu hii imefafanua kwa kina jinsi mabadiliko hayo yalivyotokea katika viwango mbalimbali vya kimuundo na kimatumizi. Matokeo yaliyowasilishwa katika sehemu hii yanaonyesha ushahidi mahsusi wa kihistoria unaothibitisha mabadiliko hayo. Hivyo yanatoa msingi wa kuelewa namna michakato ya kimaendeleo ya lugha ilivyochangia katika kubadilisha mfumo wa viambishi tamati vya vitenzi vya Kiswahili. Mabadiliko hayo yanaelezwa kama ifuatavyo:

5.4.1 Mabadiliko ya Matumizi ya KiambishiTamati {-eni} katika Vitenzi Kuonesha Wingi

Kiswahili cha kati ya mwaka 1870 hadi 1970 kilikuwa na matumizi ya kiambishi tamati {-eni} katika mazingira mapana zaidi kuliko ilivyo katika Kiswahili cha baada ya 1970. Katika baadhi ya vitenzi, {-eni} kilitumika mwishoni mwa kitenzi kuashiria wingi wa mpokeaji au mlengwa wa tendo, hususan katika miundo ambayo leo huwakilishwa kwa kutumia kiambishi yambwa {wa-} kabla ya mzizi. Hivyo, mabadiliko haya hayapaswi kuelezwa tu kama kupotea kwa {-eni}, bali kama kubadilika kwa nafasi ya kiashiria cha wingi kutoka baada ya mzizi kwenda kabla ya mzizi. Jedwali 4 unaonesha mabadiliko haya.

Na	**Kabla ya Mabadiliko**	**Baada ya Mabadiliko**
i	Ku-ku-ambi-eni	Ku-wa-ambi-a
ii	Ku-ku-it-eni	Ku-wa-it-a
iii	Ku-ku-fany-i-eni	Ku-wa-fany-i-a
iv	Ku-ku-elez-eni	Ku-wa-elez-a
v	A-li-ku-li-li-eni	A-li-wa-li-li-a
vi	A-li-ku-pig-i-eni	A-li-wa-pig-i-a
vii	A-ta-ku-kimbiz-eni	A-ta-wa-kimbiz-a
viii	A-ta-ku-chez-e-eni	A-ta-wa-chez-e-a
ix	Wa-li-ku-som-e-eni	Wa-li-wa-som-e-a
x	A-me-ku-on-esh-eni	A-me-wa-on-esh-a
xi	M-ta-wa-lim-i-eni	M-ta-wa-lim-i-a
xii	Ni-ta-ku-tengenez-e-eni?	Ni-ta-wa-tengenez-e-a

Jedwali 4:1 Mabadiliko ya Matumizi ya KiambishiTamati {-eni} katika Vitenzi Kuonesha Wingi

Chanzo: *Habari za Leo,* (Disemba 1949:3, Agosti 1951:1), *Kiongozi,* (Aprili 1906:2, 3; Januari 1910:4), *Lengo,* (Januari 1968:8), *Mambo Leo,* (Januari 1923:3, 4 na 7, Februari 1925:5), *Msimulizi,* (Oktoba 1890:3)

Mifano katika jedwali 4 inaonesha kufinyika kwa mazingira ya matumizi ya kiambishi {-eni}. Katika baadhi ya matini za Kiswahili za kipindi cha 1870 hadi 1970, kiambishi hiki kilijitokeza mwishoni mwa kitenzi kuonesha wingi wa walengwa wa tendo hata katika mazingira yasiyo ya amri, kama inavyoonekana katika *kukuambi-eni* na *kukuit-eni*. Katika Kiswahili sanifu cha sasa, dhima hiyo huwasilishwa zaidi na kiambishi cha yambwa {wa-} kinachotokea kabla ya mzizi, na hivyo kutoa maumbo *ku-wa-ambi-a* na *ku-wa-it-a*. Kiambishi {-eni}, kwa upande mwingine, kimedumisha zaidi dhima ya kuonesha wingi katika vitenzi vya amri, kama vile *nendeni*, *fanyeni*, *someni* na *andikeni*. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, hali hii inaonesha ubainishaji upya wa dhima na nafasi za viambishi katika muundo wa kitenzi: {wa-} hutumika kama kiambishi cha yambwa cha wingi kabla ya mzizi, ilhali {-eni} hutumika zaidi kama kiambishi tamati cha amri ya wingi. Kwa hiyo, mabadiliko yaliyotokea hayahusu kutoweka kwa {-eni}, bali kupungua kwa wigo wake wa matumizi na kuimarika kwa mgawanyo wa dhima baina yake na {wa-}. Uchanganuzi wake unajitokeza kama ifuatavyo:

[ambia]T
[ku[ku[ambia]eni]]T, wingi, Nfs2
[ku[wa[ambia]]]T, wingi, Nfs2: Ubadilishaji wa {ku} na {-eni} kuwa {wa} kuonyesha wingi nafsi ya pili. "kuwaambia"

Kwa hiyo, mabadiliko ya {-eni} yanaweza kuelezwa kama sehemu ya mchakato mpana wa usanifishaji wa Kiswahili, ambapo viambishi vilivyokuwa na matumizi mapana na yasiyotabirika vilipunguziwa wigo wa matumizi, huku viambishi vingine kama {wa-} vikipewa nafasi mahsusi katika muundo wa kitenzi. Hii inaonesha kuwa mabadiliko ya kimofolojia hayahusu kupotea kwa viambishi

pekee, bali pia upangaji upya wa kazi na nafasi za viambishi katika mfumo wa lugha.

5.4.2 Mabadiliko ya Kuacha Kutumia Kiambishi {ni} Mwishoni mwa Kitenzi Kuuliza Swali

Katika Kiswahili cha kati ya mwaka 1870 hadi 1970 kulikuwa na matumizi ya kiambishi {-ni} mwishoni mwa baadhi ya vitenzi kwa madhumuni ya kuuliza swali. Katika mfumo huo, dhima ya kuuliza swali iliambikwa ndani ya kitenzi chenyewe, jambo linaloonesha kuwa uulizaji wa aina hii ulikuwa na msingi wa kimofolojia. Hata hivyo, katika Kiswahili cha baada ya mwaka 1970, matumizi haya yamepungua na nafasi yake kuchukuliwa na muundo wa kisintaksia unaotumia kitenzi pamoja na kiulizi huru *nini*. Hivyo, mabadiliko haya yanaonesha kuhama kwa dhima ya swali kutoka ndani ya neno kwenda katika muundo wa sentensi. Mabadiliko haya yamejidhihirisha katika

Data katika Jedwali 5 inaonesha kuwa maumbo kama *atapata-ni?*, *amefanya-ni?*, *wataka-ni?*, *walia-ni?* na *nawaambia-ni?* yalitumika katika Kiswahili cha awali kuuliza swali. Katika maumbo haya, {-ni} kilijitokeza mwishoni mwa kitenzi kizima na kubeba dhima ya kuuliza “nini”. Hii inaonesha kuwa swali lilikuwa limefungamanishwa na muundo wa kitenzi badala ya kujitokeza kama neno huru katika tungo. Katika Kiswahili cha baada ya mwaka 1970, maumbo hayo yamebadilika na kuwa *atapata nini? amefanya nini? unataka nini? unalia nini?* na *ninawaambia nini?* Mabadiliko haya yanaonesha kuwa dhima ya kuuliza swali haikupotea, bali ilibadili nafasi yake ya kimuundo. Awali, dhima hiyo iliwakilishwa na kiambishi ndani ya kitenzi; baadaye, imewakilishwa na kiulizi huru *nini* kinachojitokeza baada ya kitenzi. Kwa hiyo, mabadiliko haya yanaweza kuelezwa kama uhamaji kutoka uundaji wa swali wa kimofolojia kwenda uundaji wa swali wa kisintaksia. Kwa nadharia ya Mofolojia Leksika, data hii inachanganuliwa kama ifuatavyo:

[pata]T
[a[ta[pata]]]T, umoja, Nfs3
[[a[ta[pata]]]ni?]T, umoja, Nfs3, swali: Upachikaji wa {ni} mwishoni kuashiria swali”
[[a[ta[pata]]]T, umoja, Nfs3: udondoshaji wa {-ni} ya swali “atapata”.
Nje ya leksikoni: “atapata nini?

Aidha, mabadiliko haya yanaweza kueleweka kama sehemu ya mchakato mpana wa kusawazisha mfumo wa Kiswahili. Mfumo wa kutumia *nini* kama neno huru unaweka wazi zaidi mipaka kati ya kitenzi na kipashio cha kuuliza swali. Kwa msingi huo, kuacha kutumia {-ni} mwishoni mwa kitenzi kunaonesha si kupotea kwa maana ya swali, bali kupanga upya namna maana hiyo inavyowasilishwa katika muundo wa lugha kama inavyojitokeza katika Jedwali 5.

Na	**Kabla ya Mabadiliko**	**Baada ya Mabadiliko**
I	Atapata-**ni**?	Atapata **nini**?
Ii	Amefanya-**ni**?	Amefanya **nini**?
Iii	Wataka-**ni**?	Unataka **nini**?
Iv	Walia-**ni**?	Unalia **nini**?
V	Nawaambia-**ni**?	Ninawaambia **nini**?
Vi	Mnasema-**ni**?	Mnasema **nini**?
Vii	Mnakimbia-**ni**?	Mnakimbia **nini**?

Jedwali 5: Mabadiliko ya Kuacha Kutumia Kiambishi {ni} Mwishoni mwa Kitenzi Kuuliza Swali
Chanzo: Steere (1870:122)

5.4.3 Mabadiliko ya Nafasi ya Viambishi vya Urejeshi

Katika Kiswahili cha kati ya mwaka 1870 hadi 1970, viambishi vya urejeshi vilijitokeza mara nyingi baada ya mzizi wa kitenzi. Hali hii ni tofauti na Kiswahili cha baada ya mwaka 1970, ambapo viambishi hivyo hujitokeza zaidi kabla ya mzizi, hasa baada ya kiambishi cha njeo au hali. Mabadiliko haya yanaonesha uhamaji wa nafasi ya viambishi vya urejeshi kutoka katika nafasi ya baada ya mzizi kwenda katika nafasi ya kabla ya mzizi. Kwa mtazamo wa kimofolojia, uhamaji huu unaashiria upangaji upya wa vipashio vya kitenzi ili kuweka uwazi zaidi katika nafasi na dhima ya kiambishi cha urejeshi. Data katika Jedwali 6 (i-xvi) inadhihirisha mabadiliko haya.

Na	**Kabla ya Mabadiliko**	**Baada ya Mabadiliko**
I	Waitumia-**o**	Wana-**o**-itumia
Ii	Waagiza-**o**	Wana-**o**-agiza
Iii	Yafaa-**yo**	Yana-**yo**-faa
Iv	Yakaa-**yo**	Yana-**yo**-kaa
V	Aendesha-**ye**	Ana-**ye**-endesha
Vi	Am-lea-**ye**	Ana-**ye**-mlea
Vii	Vieleza-**vyo**	Vina-**vyo**-eleza
Viii	Aenda-**vyo**	Ana-**vyo**-enda
Ix	Kifanywa-**cho**	Kina-**cho**-fanywa
X	Kipelekwa-**cho**	Kina-**cho**-pelekwa
Xi	Watoka-**po**	Wana-**po**-toka
Xiii	Walala-**po**	Wana-**po**-lala
Xiv	Wajenga-**zo**	Wana-**zo**-jenga
Xv	Zitushinda-**zo**	Zina-**zo**-tushinda
xvi	Wafanya-**lo**	Wana-**lo**-fanya
xviii	Lionyesha-**lo**	Lina-**lo**-onyesha

*Jedwali 6: **Mabadiliko ya Nafasi ya Viambishi vya Urejeshi***
Chanzo: *Bendera ya Kikristo,* (Novemba 1948:6, 1948:8; Novemba 1949:8; Januari 1950:1 na 4, Januari 1950:8, Januari 1952:1, Mei 1951:7, Februari 1952:7, Juni 1954:4);*Habari za Leo,* (Agosti 1951:4), *Kiongozi*, (Aprili 1906:2, Agosti 1908:1 na 2) *Lengo,* (Januari, Machi 1966:9, *Lengo*, Januari 1968:4,

1968:7, Aprili 1969:9), *Mambo Leo,* (Februari 1925:4, Februari 1925:3, Disemba,1929:4, Januari 1931:2 na 7, Disemba 1953:3); *Mwafrika*, (Machi 1964:5); *Umoja*, (Julai 1962:1 na 4, 1962:3, Julai 1962:1, Disemba 1961:4)

Data katika Jedwali 6 zinaonesha kuwa katika matini za Kiswahili za mwaka 1870–1970, viambishi vya urejeshi {-o}, {-yo}, {-ye}, {-vyo}, {-cho}, {-po}, {-zo} na {-lo} vilijitokeza baada ya mzizi. Maumbo *waitumiao, waagizao, yafaayo, aendeshaye, aendavyo, kifanywacho, watokapo, wajengazo* na *wafanyalo* yanathibitisha mpangilio huo. Hata hivyo, muundo huu haujatoweka katika Kiswahili cha sasa; maumbo *aendaye, asemaye, wafanyao, kifanywacho* na *waendapo* bado yanatumika sambamba na *anayeenda, anayesema, wanaofanya, kinachofanywa* na *wanapoenda*. Hakimu (2020, 2023) anaeleza kuwa Kiswahili hutumia mikakati yote miwili ya urejeshi.
Pamoja na matumizi hayo sambamba, muundo unaoweka kiambishi cha urejeshi kabla ya mzizi umeimarika katika Kiswahili sanifu, hasa katika vitenzi vyenye alama dhahiri ya njeo au hali. Katika muundo huo, urejeshi hutokea baada ya kiima na njeo au hali, lakini kabla ya yambwa na mzizi. Kwa mfano, *wanaoitumia* huchanganuliwa kuwa *wa-na-o-i-tumi-a*: {wa-} ni kiima, {-na-} ni njeo, {-o-} ni urejeshi, {-i-} ni yambwa, {-tumi-} ni mzizi na {-a} ni irabu ya mwisho.

Mpangilio huu unaendana na kiolezo cha kitenzi cha Kibantu cha Meeussen (1967) na maelezo ya Nurse (2003, 2008):

Kiima + Njeo/Hali + Urejeshi + Yambwa + Mzizi + Viambishi-tamati + Irabu-mwisho.
Chanzo: (Meeussen, 1967; Nurse, 2003; Hakimu, 2020, 2023).

Kiolezo hiki kinaonesha kuwa kila kiambishi huchukua nafasi maalumu kulingana na dhima yake ya kisarufi. Hivyo, mabadiliko yaliyobainika hayamaanishi kutoweka kwa muundo unaoweka kiambishi cha urejeshi baada ya mzizi, bali yanaonesha kuimarika na kusanifishwa kwa muundo unaokiweka kabla ya mzizi. Muundo huu huonesha kwa uwazi zaidi uhusiano kati ya kiima, njeo au hali, urejeshi, yambwa na mzizi wa kitenzi. Kwa hiyo, matumizi sambamba ya miundo *waitumiao* na *wanaoitumia* yanaonesha mwendelezo wa kihistoria na mabadiliko ya kimofolojia katika Kiswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, umbo *wanaoitumia* hujengwa kitabaka kama ifuatavyo:

[tumia]T
[i[tumia]]]T, umoja, Nfs3
[[wa[i[tumia]]o]T, wingi, Nfs3, urejeshi
[wa[na[o[i[tumia]]]]]T, wingi, Nfs3, urejeshi
"wanaoitumia".

Uchanganuzi huu unathibitisha kuwa mofimu za kitenzi huongezwa kwa hatua zinazofuatana na kwamba kila hatua huunda umbo jipya lenye taarifa mahususi ya kisarufi. Hivyo, kuimarika kwa muundo *wanaoitumia* kunaakisi mwelekeo wa Kiswahili wa kusawazisha mpangilio wa viambishi na kuweka wazi dhima ya kila mofimu katika muundo wa kitenzi.

6.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza mabadiliko ya maumbo ya vitenzi vya Kiswahili katika matini rasmi za mwaka 1870–1970. Matokeo yamebaini mabadiliko ya viambishi vya kabla na baada ya mzizi, yakiwamo {twa-}, {mwa-} na {wa-} kuwa {tu-}, {m-} na {u-}; kuimarika kwa {-na-} ya wakati uliopo; kubadilika kwa {mw-} kuwa {mu-} kabla ya irabu /u/; kupungua kwa matumizi mapana ya {-eni}; kutoweka kwa {-ni} mwishoni mwa kitenzi katika maswali; na kuhamia kwa viambishi vya urejeshi kutoka baada ya mzizi kwenda kabla yake. Mabadiliko haya hayakuwa ya kiholela, bali yaliakisi upangaji upya, urahisishaji na usawazishaji wa mfumo wa kimofolojia. Aidha, kuongezeka au kuhamishwa kwa viambishi kulibadili idadi na mpangilio wa silabi, hivyo kuathiri mahali pa mkazo katika baadhi ya vitenzi. Hali hii inathibitisha uhusiano wa karibu kati ya mofolojia na fonolojia. Vilevile, usanifishaji uliimarisha mpangilio thabiti wa viambishi na kukiwezesha Kiswahili kukua kama lugha ya mawasiliano rasmi, elimu, utawala na matumizi mapana ya kijamii.

7.0 Mapendekezo

Makala hii inapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanyike kuhusu mabadiliko ya kimofolojia katika aina nyingine za maneno kama vile nomino, vivumishi, vielezi na viwakilishi. Aidha, tafiti zijazo zinaweza kuchunguza uhusiano kati ya mabadiliko ya kimofolojia na mabadiliko ya kifonolojia au kisintaksia katika Kiswahili. Vilevile, kuna umuhimu wa kufanya tafiti linganishi kati ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ili kubaini kama mabadiliko yaliyobainishwa katika makala hii ni ya Kiswahili pekee au ni sehemu ya mienendo mipana ya mabadiliko katika lugha za Kibantu.

Marejeleo

Aronoff, M. (1976). *Word formation in generative grammar*. MIT Press.

Babusa, H. (2019). Ukopaji wa lugha: Etimolojia na mabadiliko ya maana na utamkaji wa msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili. *International Journal of Advanced Research, 7*(9), 101-105.

Batibo, H. M. (2002). The evolution of the Kiswahili syllable structure. *South African Journal of African Languages, 22*(1), 1-10.

Bendera ya Kikristo. (1947-1959). Lushoto, Tanzania: Lutheran Mission Press.

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa lugha na isimu*. Dar es Salaam University Press.

Gibson, H., Mapunda, G., Marten, L., Shah, S., & Taji, J. (2019). Variation in double object marking in Swahili. *Swahili Forum, 26*, 142-165.

Gichuru, T. M. (2020). *Mabadiliko ya maana za leksia za Kiswahili: Mtazamo linganishi wa kikale na kisasa* (Tasinifu ya uzamivu haijachapwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Habari za Leo. (1945-1956). Dar es Salaam, Tanganyika Territory.

Hakimu, J. (2020). *Ubantuishaji wa kimofolojia katika vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu* [Tasnifu ya uzamivu ambayo haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hakimu, J. (2020). *Ubantuishaji wa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu* (Tasinifu ya uzamivu haijachapwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hakimu, J. (2023). Ruwaza ya vitenzi vya Kibantu katika muktadha wa vitenzi vya Kiswahili. *Nuru ya Kiswahili, 2*(2), 49-73.

Hans, M. M. (2017). Usanifishaji wa Kiswahili Afrika Mashariki: Changamoto na namna ya kukabiliana nazo. *JULACE: Journal of the University of Namibia Language Centre, 2*(2), 100–121.

Hussein, H. A. (2016). *Mabadiliko ya kifonolojia na kisemantiki katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu* [Tasnifu ya uzamivu ambayo haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Katamba, F., & Stonham, J. (2018). *Morphology* (2nd ed.). Bloomsbury Academic.

Kiongozi. (1910-1916). Dar es Salaam, Tanganyika Territory: Evangelical Missions.

Kipacha, A. (2005). An ethno-linguistic perspective on Kingome Swahili narrative texts. *Nordic Journal of African Studies, 14*(3), 356-367.

Kiparsky, P. (1982). Lexical morphology and phonology. In I.-S. Yang (Ed.), *Linguistics in the morning calm: Selected papers from SICOL-1981* (3–91). Hanshin Publishing Company.

Lengo. (1964-1970). Dar es Salaam & Nairobi, Kenya: East African Venture Ltd.

Lieber, R. (1992). *Deconstructing morphology: Word formation in syntactic theory*. University of Chicago Press. Taarifa za kitabu

Mambo Leo. (1923-1964). Dar es Salaam, Tanganyika Territory.1q

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya usanifishaji wa Kiswahili*. TUKI.

Meeussen, A. E. (1967). Bantu grammatical reconstructions. *Africana Linguistica, 3*, 79-121. https://doi.org/10.3406/aflin.1967.873

Msimulizi. (1888-1914). Zanzibar: Universities' Mission to Central Africa (UMCA).

Mwaro-Were, G. A. W. (2001). Uundaji wa istilahi za Kiswahili zenye ukubalifu wa kimataifa. *Journal of the Department of Languages, Makerere University, Uganda*.

Ngonyani, D. S. (2006). Lexical innovation in Tanzania's political discourse. *Kiswahili, 69*, 1-29.

Nurse, D. (2003). Aspect and tense in Bantu languages. In D. Nurse & G. Philippson (Eds.), *The Bantu languages* (90-102). Routledge.

Nurse, D. (2008). *Tense and aspect in Bantu*. Oxford University Press.

Nurse, D., & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A linguistic history*. University of California Press.

Petzell, M. (2005). Expanding the Swahili vocabulary. *Africa and Asia, 5*, 85-107. www.sprak.gu.se/digitalAssets/1307/130769-petzell-expanding.pdf

Polome, E. C. (1967). *Swahili language handbook*. Center for Applied Linguistics.

Pwani na Bara. (1910-1916). Dar es Salaam, Tanzania: Evangelical Lutheran Church in Tanzania.

Schönhof-Wilkans, A. (2012). On the question of transitive and intransitive verbs in

Swahili. *Lingua Posnaniensis, 54*(1), 89-97.

Shembilu, M. M. (2015). Mapokeo ya kisemantiki ya nomino za mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. *Kioo cha Lugha, 13*, 144-156.

Steere, E. (1870). *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. Bell & Daldy.

Ud Deen, K. (2005). *The acquisition of Swahili*. John Benjamins Publishing Company.

Umoja. (1947-1962). Moshi, Tanzania: Lutheran Mission Press.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha mofolojia ya Kiswahili*. TATAKI.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Descriptive issues in Kiswahili verbal structure*. www.kab.ac.ug/...descriptive-issues-in-Kiswahili-verbal-structure.